

Watu kumi wahukumiwa kifo Msumbiji

Na Accadoga Chileli,
Maputo

WATU kumi walihukumiwa adhabu ya kifo na mahakama ya kijeshi ya mapinduzi baada ya kupatikana na hatia ya kuhatarisha usalama wa wananchi wa Msumbiji.

Mzalendo 15/4/79

Wote kwa pamoja walipatikana na hatia ya ujasusi, upelelezi na ugaidi kwa nchi ya Msumbiji. Taarifa iliyotolewa na mahakama hayo ilisema kuwa watu hao walichukua mafunzo ya ugaidi kutoka kwa walowezi wa Zimbabwe.

Watu waliouawa ni Robi Joaquim Pereira, Armando Mavinha Naposse, Frengue Chilengue, Josefa Naposse, Lee Chuan na Conjane Francisco Zinotenga wote wakiwa raia wa Msumbiji. Wengine ni Yum Rumesso Magazine, Nhimiode Jena, Namo Macopa na Zadrique Sithole ambao wanatoka Zimbabwe.

Watu kumi wengine, saba kati ya hao wakiwa ni raia wa Msumbiji, wawili kutoka Zimbabwe na mmoja raia wa Ureno walihukumiwa adhabu ya kifo na kuuawa kwa kupigwa risasi Machi 31.

Mahakama ya kijeshi ya Msumbiji itakuwa ikisimamia kesi za namna hiyo mpaka hapo mahakama kuu itakapoanzishwa.